JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

## TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

# MWONGOZO WA HATUA ZA NIDHAMU NA RUFAA KWA WALIMU

**Toleo Na.1, 2017**

# MWONGOZO WA HATUA ZA NIDHAMU NA RUFAA KWA WALIMU

**Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia Sheria ya Tume ya Utumishi Wa Walimu Na. 25 Ya 2015, Kanuni zake za 2016, Kanuni za Utumishi wa Umma za 2003 na Kanuni za Utendaji Bora wa Masuala ya Nidhamu za katika Utumishi wa Umma za 2007**

## MWONGOZO UMETOLEWA NA:

**Tume ya Utumishi wa walimu,**
**S.L.P 353**
**DODOMA**
**SIMU: 026 -2322402**
**Tovuti: www.tsc.go.tz**
**Baruapepe: secretary@tsc.go.tz**

## 1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu ni maelekezo mahsusi kwa Mamlaka ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu ambayo ni [*Tume ya Utumishi wa Walimu* (TSC) *ngazi ya Wilaya na Makao Makuu*] kuhusu hatua wanazopaswa kuzingatia wakati wa kutekeleza majukumu yao yaliyoainishwa chini ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume na Kanuni hizo, Tume ni Mamlaka ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu wa Shule ya Msingi na Sekondari za Umma, Tanzania Bara [*Kifungu cha 4 na 5(c)*]. Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 12(5) ya Kanuni za Tume za mwaka 2016, Mamlaka za Nidhamu kwa Walimu zimeamriwa kusimamia uzingatiaji wa Taratibu za kinidhamu zilizoainishwa na Sheria ya Tume na Kanuni zake, na au Taratibu au Miongozo itakayoandaliwa na Tume.

Aidha, Mamlaka hizo pia zinapaswa kuzingatia Taratibu za Uendeshaji wa Walimu za mwaka 2016, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, pamoja na Nyaraka mbalimbali

za Kiutumishi ambazo ni nyezo muhimu katika kusimamia Utumishi wa Walimu.

## 2.0 WATEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU

Wafuatao ni watekelezaji wakuu wa Mwongozo huu.

(i) Watumishi wa Tume (TSC) ngazi ya Makao Makuu,
(ii) Makatibu Wasaidizi wa Tume ngazi ya Wilaya,
(iii) Wajumbe wa Kamati za Nidhamu za Tume ngazi ya Wilaya,
(iv) Wakuu wa Shule za Sekondari, na
(v) Walimu Wakuu wa Shule za Msingi

Aidha, waajiri (*Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji*) pamoja na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Umma, wanashauriwa kupitia mwongozo huu ili wajue Taratibu za kinidhamu na Rufaa zinazopaswa kuzingatiwa kwenye utumishi wa Walimu.

## 3.0 MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

Zifuatazo ni Mamlaka za Nidhamu kwa Walimu kwa mujibu wa *Kanuni ya 46(1) na 12(2)(3)* ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016.

(i) **Kamati ya Wilaya** (*Ajira, Upandishwaji vyeo na Nidhamu*)

(ii) **Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu.**

**Angalizo;** Kwa mujibu wa *Kanuni ya 12(1)* Tume (Makao makuu) inayo Mamlaka ya kusimamia mashauri ya Nidhamu dhidi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walioajiriwa kwenye Utumishi wa Umma.

## 4.0 MAMLAKA ZA RUFAA KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

Zifuatazo ni Mamlaka za Rufaa kwa Walimu kwa mujibu wa *Kifungu cha 13* cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015.

(i) **Kamati ya Wilaya**

Kwa Walimu wanaopinga uamuzi wa kinidhamu uliofanywa na Wakuu wa Shule [*Kifungu 13(1)*]

(ii) **Tume ya Utumishi wa Walimu (Makao Makuu)**
Kwa Walimu wanaopinga uamuzi wa Kamati ya Wilaya[*Kifungu 13(2)*]

(iii) **Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
Kwa Walimu wanaopinga uamuzi wa Tume ya Utumishi wa Walimu -Makao Makuu. *[Kifungu cha 13(3)]*

## 5.0 MWENENDO WA MAKOSA YA NIDHAMU NA ADHABU ZAKE.

Zifuatazo ni aina mbili za mwenendo wa kufuata/kuzingatia wakati wa kuchukua hatua za Nidhamu kwa Walimu [*Kanuni ya 13(1)(2)(4)*].

(i) **Mwenendo wa Makosa Mazito** (*Formal proceedings*)

Mwenendo huu unatumika pale ambapo Mamlaka ya Nidhamu inaona kosa

alilotuhumiwa Mwalimu kutenda, lina uzito unaowezesha apewe moja kati ya adhabu zifuatazo; [*Kanuni ya 13(2) na 15*]

- Kufukuzwa kazi
- Kushushwa cheo/daraja
- Kupunguzwa mshahara
- Kusimamishiwa nyongeza ya mshahara

(ii) **Mwenendo wa Makosa Mepesi** [*Summary proceedings*]

Mwenendo huu unatumika pale ambapo Mamlaka ya Nidhamu inaona kosa alilotuhumiwa Mwalimu kutenda na baada ya kutiwa hatiani, halina uzito unaowezesha apewe moja kati ya adhabu zifuatazo; *Kanuni ya 13(4) na 20*]

- Kufukuzwa kazi
- Kushushwa cheo/daraja
- Kupunguzwa mshahara
- Kusimamishiwa nyongeza ya mshahara

**Angalizo:** Katika mwenendo wa makosa mepesi, Mwalimu aliyetiwa hatiani atapewa moja kati ya adhabu zifuatazo:-
[*Kanuni ya 12(3)*]

(i) Kufidia hasara au sehemu ya hasara iliyosababishwa na makosa au uzembe.

(ii) Kushikilia nyongeza za mshahara

(iii) Karipio

(iv) Onyo

## 6.0 MAKOSA YA NIDHAMU

### 6.1 Orodha ya makosa ya Nidhamu yanayochukuliwa hatua kwa mwenendo wa makosa mazito

[*Kanuni ya 11(1)*]

(a) Kutenda au kuacha kutenda jambo kinyume na dhamiri au Tabia njema ya Utumishi wa Umma ikiwemo wizi, ubadhirifu, n.k.;

(b) Kutenda au kuacha kutenda jambo linalosababisha Utumishi wa Walimu usiheshimike;

(c) Ukaidi/dharau (insubornation);

(d) Kutokuwa kazini zaidi ya siku tano bila ruhusa au sababu za msingi;

(e) Matumizi mabaya ya Mamlaka au rasilimali iliyotolewa kwa ajili ya Utumishi wa Walimu;

(f) Kujihusisha na shughuli zozote (nje ya kazi za ofisi) zenye faida kwa kutumia cheo cha mhusika kwenye utumishi wa Walimu;

(g) Kukataa uhamisho;

(h) Kushindwa kutekeleza majukumu aliyopewa;

(i) Kuvujisha taarifa za siri kinyume na Sheria ya Usalama wa Taifa;

(j) Kutenda au kuacha kutenda jambo kinyume na maslahi ya Umma;

(k) Kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo kwa sababu za matumizi ya pombe au dawa za kulevya;

(l) Uzembe uliosababisha hasara kwa Mwajiri;

(m) Uzembe mkubwa wa kutotekeleza majukumu;

(n) Kukiuka:-

(i) Maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa Walimu yaliyoainishwa na Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu; na

(ii) Maadili ya Taaluma na utendaji kazi au Maadili ya Uongozi wa Umma yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma.

6.2 **Orodha ya makosa ya Nidhamu yanayochukuliwa hatua kupitia mwenendo wa makosa mepesi**
[*Kanuni ya 11(2)]*

(a) Kuchelewa kazini bila ruhusa au sababu za msingi;

(b) Kutokuwepo mahali pa kazi nyakati za kazi bila ruhusa;

(c) Kutokuwepo kazini bila ruhusa;

(d) Kushindwa kukamilisha kazi;

(e) Uzembe wa kutotekeleza majukumu yasiyoathiri usalama wa mtu au mali; na

(f) Kushindwa kuzingatia maelekezo yasiyosababisha ukaidi/dharau (insubornation)

## 7.0 UWEZO WA MAMLAKA ZA NIDHAMU KUTOA ADHABU

**(i) Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu**

Wameruhusiwa kutoa adhabu zifuatazo tu: [*Kanuni ya 12(3)]*

- Kufidia hasara au sehemu ya hasara iliyosababishwa na makosa au uzembe;
- Kushikilia nyongeza ya mshahara
- Karipio
- Onyo

**(ii) Kamati ya Wilaya**

Imeruhusiwa kutoa adhabu zifuatazo; *(Kanuni ya 12(2)(4)*

- Kufukuzwa kazi
- Kushushwa cheo
- Kushushwa mshahara
- Kusimamisha nyongeza ya mshahara

**Angalizo:** Kamati ya wilaya pia imeruhusiwa kutoa adhabu zinazotolewa na Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kama zilivyoainishwa kwenye Kipengele cha 7.0(i) hapo juu.
[*Kanuni 12(4) na 27*]

## 8.0 HATUA ZA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU

### 8.1 Kupokea tuhuma dhidi ya Mwalimu

**(i)** Kwa kuzingatia *Kanuni ya 12(1) na 47* (a) ya Kanuni za Utumishi wa Walimu, Kamati ya Wilaya inayo Mamlaka ya kinidhamu kwa Walimu walioko kwenye Wilaya husika. Aidha, kwa kuwa Waajiri (*Wakurugenzi wa Halmashauri , Manispaa, Miji na Majiji*) ni wasimamizi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Umma kwa watumishi hao, wanalo jukumu la kuwasilisha taarifa (tuhuma) za ukiukwaji wa Miongozo hiyo kwa Mamlaka ya Nidhamu (Tume ngazi ya Wilaya) ili hatua za Nidhamu zichukue mkondo wake.

(ii) Kwa msingi huo, Katibu Msaidizi wa Tume ngazi ya Wilaya ambaye ni msimamizi wa Utumishi wa Walimu katika wilaya husika, anapaswa kuanzisha mchakato wa kinidhamu baada ya kupokea kutoka kwa Mwajiri barua yenye tuhuma za ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu, pamoja na ushahidi wake.

(iii) Ili Waajiri waweze kuwasilisha tuhuma zilizo sahihi, Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu wanalo jukumu la kushirikiana na Waajiri kwa kuwapa maelezo na vielelezo mbalimbali vya kuthibitisha tuhuma za makosa mazito yaliyoainishwa kwenye **Kipengele cha 6.1** cha Mwongozo huu.

(iv) Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu wanaaswa kutowasilisha tuhuma za ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu moja kwa moja kwenda kwa Mamlaka ya Nidhamu bila kupitisha kwa **Mwajiri** ili ajiridhishe (*na siyo kuwasilisha tuhuma kwa Afisa Elimu pekee*).

**(v)** Vivyo hivyo, Mamlaka ya Nidhamu haipaswi kuanzisha mchakato wa Nidhamu dhidi ya Mwalimu kutokana na tuhuma zilizotolewa na Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu pasipo kupitishwa na Mwajiri.

**(vi)** Mwajiri na Mamlaka za Nidhamu wazingatie mambo yafuatayo wakati wa kuwasilisha au kupokea tuhuma za Nidhamu:-

- Barua ya kuwasilisha tuhuma itaje majina ya mtuhumiwa yanayotumika kwenye ajira yake.

- Kuwe na taarifa ya aina ya kosa alilotenda mtuhumiwa, muda, mahali, na mazingira ya kosa lilivyofanyika.

- Barua ya kuripoti tuhuma iambatane na vielelezo muhimu vya ushahidi wa tuhuma kama vile; daftari la mahudhurio (*lenye mhuri wa mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu*), hati za matibabu, barua za ruhusa n.k.

- Barua ya Mwajiri ya kuripoti tuhuma kwa Mamlaka ya Nidhamu iambatane na

taarifa ya Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu juu ya tuhuma za mwalimu kutenda kosa la kinidhamu katika Shule husika.

- Barua ya kuripoti tuhuma iwe imesainiwa na Mwajiri. Tofauti na Mwajiri, mtumishi yeyote aliyesaini barua hiyo kama Afisa Utumishi au Afisa Elimu (*pasipo idhini ya Mwajiri*) haitatafsiriwa kuwa tuhuma zimetoka kwa Mwajiri.

**<u>ANGALIZO:</u>** **Jedwali la Kwanza (linalofuata) lisomwe kwa "Columns"(anza juu-chini); Jedwali la Pili na la Tatu yasomwe kwa "Rows" (anza kushoto – kulia)**

**JEDWALI LA 1:**

## MAJUKUMU NA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA HATUA ZA NIDHAMU

| JUKUMU | HATUA ZA KUTEKELEZA | REJEA YA SHERIA | MTEKELEZAJI | MAMBO YA KUZINGATIA |
|---|---|---|---|---|
| **KUFANYA UCHUNGUZI WA AWALI** | ▪ Kupitia (kusoma) majalada na taarifa mbalimbali zinazohusu tuhuma.<br>▪ Kuhoji watu (kupata maelezo) kuhusu mtuhumiwa<br>▪ Kukusanya vielelezo<br>▪ Kuandaa taarifa ya uchunguzi wa awali dhidi ya tuhuma husika | ▪ **Kanuni ya 15(2)** *(Kanuni za Tume ya utumishi wa Walimu, 2016)*<br>▪ **Kipengele cha 10.0 na 11.0** *(Taratibu za Uendeshaji Bora wa masuala ya Nidhamu, ,2007)*<br>▪ **Kanuni ya 37** *(Kanuni za utumishi wa umma, 2003)* | Mamlaka ya Nidhamu | ▪ Kubaini usahihi wa tuhuma zilizotolewa dhidi ya mtumishi.<br>▪ Kubaini kama kuna ulazima na ushahidi wa kuchukua hatua za Nidhamu kwa kutoa adhabu.<br>▪ Iwapo tuhuma zitakuwa na ushahidi wa kutosha, Mamlaka ya Nidhamu itaanzisha shauri la Nidhamu kwa kuzingatia **uzito wa kosa.**<br>▪ Mtuhumiwa anaweza **kupumzishwa kazi (Relieve of duties administratively )** bila kuathiri<br>▪ mishahara/ maslahi yake, wakati wa kufanya uchunguzi. |

| JUKUMU | HATUA ZA KUTEKELEZA | REJEA YA SHERIA | MTEKE LEZAJI | MAMBO YA KUZINGATIA |
|---|---|---|---|---|
| **KUANZISHA SHAURI LA NIDHAMU** | kuchagua mwenendo wa makosa. Ikiwa ni wa makosa mazito (*formal proceedings*) au Makosa mepesi (*Summary proceedings*) mtuhumiwa apewe Hati ya Mashtaka na Notisi yenye maelezo ya kumtaka atoe utetezi wake (na siyo barua), | **Kanuni ya 15** na **20** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu- 2016)* | Mamlaka ya Nidhamu (*ngazi ya Shule na Wilaya*) | ▪ Hati ya Mashtaka na Notisi viandaliwe kwa kuzingatia matakwa ya **Jedwali la Pili, Sehemu A na B** ya Kanuni za *Tume ya Utumishi wa Walimu- 2016* .<br>▪ Makosa anayotuhumiwa kutenda Mwalimu yawe wazi na yaendane na makosa yaliyotajwa kwenye Sheria/ Kanuni.<br>▪ Hati ya mashtaka isainiwe na Mamlaka ya Nidhamu yenyewe au aliyekasimiwa Mamlaka hayo.<br>▪ Anuani au njia sahihi na yenye uhakika itumike kufikisha Hati ya Mashtaka kwa mtuhumiwa na kuwe na ushahidi wa Hati kutumwa kwa mlengwa.<br>▪ Kuwe na maelezo ya kuridhisha endapo mtuhumiwa hakupokea Hati ya mashtaka.<br>▪ Mamlaka ya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Nidhamu (inapobidi) inaweza kuomba ushauri kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali jinsi ya kuandaa Hati ya Mashtaka<br><br>▪ Endapo itaibainika kuwa Hati ya Mashtaka (ya makosa mazito) aliyopewa mtuhumiwa imekosewa Mamlaka ya Nidhamu **haitabatilisha shauri** bali inaruhusiwa **kubadilisha** kwa kutoa Hati mpya kwa muda usiozidi **siku thelathini (30)** tangu tarehe ilipotolewa Hati ya awali (iliyokosewa) kwa mtuhumiwa.<br><br>▪ Hati ya mashtaka iliyorekebisha Hati ya awali ioneshe **kufutwa** kwa Hati ya awali.<br><br>**Kwa mwenendo wa makosa mazito (*Formal proceedings*)**<br><br>▪ Endapo shauri litakaloanzishwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | litahusu kosa la Utoro kazini zaidi ya siku 5, badala ya kukimbilia matumizi ya **Kanuni ya 28(1)** yenye adhabu moja , Mamlaka ya Nidhamu izingatie Kanuni ya **11(1)(d)** inayohusu kosa la utoro wenye adhabu tofauti/ mbadala. |
| | Kuandika barua ya Kusimamisha kazi | ▪ **Kanuni ya 14** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu- 2016*)<br><br>▪ **Kanuni ya 38** *(Kanuni za utumishi wa umma, 2003*) | Mamlaka ya Nidhamu ngazi ya Wilaya | ▪ Mamlaka ya Nidhamu, **inaweza kumsimamisha kazi** mtuhumiwa ikiridhika kuwa mtuhumiwa ana tuhuma za kujibu na kwa maslahi ya umma asiendelee kufanya kazi.<br><br>▪ Hatua ya kusimamishwa kazi siyo ya lazima bali ni hiyari au utashi wa Mamlaka ya Nidhamu ikiona inafaa na kwa maslahi ya umma.<br><br>▪ Mtuhumiwa aelezwe (kwa barua) sababu za kusimamishwa kazi<br><br>▪ Kusimamishwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | kazi kunafanywa baada ya mtuhumiwa kupewa Hati ya Mashtaka na siyo vinginevyo.<br><br>▪ Mwalimu aliyesimamishwa kazi ni **lazima** alipwe siyo chini ya nusu ya mshahara wake.<br>▪ Mishahara iliyoshikiliwa na Mwajiri irejeshwe/ilipwe kwa mtuhumiwa (Mwalimu) iwapo hatapatikana na hatia ya kosa alilotuhumiwa.<br><br>▪ Iwapo mwalimu aliyeshtakiwa amepewa adhabu yoyote tofauti na adhabu ya kufukuzwa kazi, atapaswa kurejeshewa nusu ya nusu ya mshahara ulioshikiliwa . |
| **KUUNDA KAMATI YA UCHUNGUZI** | ▪ Kuandika barua ya kumteua Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi.<br><br>▪ Kutoa hadidu | **Kanuni ya 16, 17** na **18 (10)** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu-2016*) | Mamlaka ya Nidhamu ya Wilaya | ▪ Kamati ya Uchunguzi iundwe kwa mwenendo wa **makosa mazito au Mepesi .**<br>▪ Kamati iundwe baada ya mtuhumiwa kupewa Hati ya Mashtaka na iwapo :- |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | rejea kwa Kamati ya Uchunguzi.<br><br>▪ Kukabidhi vielelezo vya ushahidi kwa Kamati ya Uchunguzi.<br><br>▪ Kuteua wataalam wa kusaidia Kamati ya Uchunguzi endapo kuna hoja ya kiufundi. | | | (i) Mtuhumiwa ameshindwa kuwasilisha utetezi wake kwa muda aliopewa;<br><br>(ii) Katika utetezi mtuhumiwa amekanusha tuhuma; au<br><br>(iii) Utetezi hauridhishi<br><br>▪ Kamati ya Uchunguzi **isiundwe** kama mtuhumiwa amekiri kutenda kosa alilotuhumiwa.<br><br>▪ Kamati iliyoteuliwa ianze kufanya kazi ndani ya **siku 60** tangu kutolewa kwa Hati ya mashtaka.<br><br>▪ Wajumbe wa Kamati wawe waadilifu, huru (*wasioegemea upande wowote*), na wenye kaliba /uwezo wa kumhoji Mwajiri na Mamlaka ya Nidhamu pamoja na mashahidi wao. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ▪ Muundo wa Kamati uzingatie:-<br><br>(i) Idadi ya wajumbe isiyozidi wa 4 na wasiopungua wa 2<br>(ii) Wajumbe wawe na cheo chanye ngazi ya Uandamizi au zaidi, au cheo/ngazi ya juu kuliko aliyonayo Mwalimu mtuhumiwa.<br>(iii) Kuwe na wajumbe wa jinsi zote (kike na kiume)<br><br>▪ Ikiwezekana Mwenyekiti wa Kamati atoke Taasisi nyingine.<br><br>▪ Barua za uteuzi wa Kamati ya Uchunguzi zieleze sababu ya uteuzi huo.<br><br>▪ Hadidu Rejea zieleweke na zilenge tuhuma husika.<br><br>▪ Vielelezo vinavyokabidhiwa kwa Kamati vihusiane na tuhuma.<br><br>▪ Kamati ikihitaji mtaalam iombe kwa Mamlaka ya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Nidhamu ambayo itawajibika kuwapata watalamu (Walimu) wasiozidi wawili. |
| **KUFANYA UCHUNGUZI** | ▪ Kamati ya Uchunguzi itume barua ya kumjulisha mtuhumiwa kuhusu siku, tarehe, muda na mahali ambapo Uchunguzi utafanyika, haki ya kuhoji , kuwakilishwa, na kuwasilisha ushahidi na mashahidi.<br><br>▪ Mwenyekiti kujitambulisha na kuwatambulisha wajumbe wa Kamati na mashaidi wa Mwajiri kwa kutaja majina na vyeo vyao.<br><br>▪ Mwenyekiti kuelezea malengo ya | **Kanuni ya 18** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu-2016*)<br><br>▪ **Kipengele cha 16.0 na 17.0** (*Taratibu za Uendeshaji Bora wa masuala ya Nidhamu, 2007*) | Kamati ya Uchunguzi | ▪ Mamlaka ya Nidhamu na Mwajiri wasiwe sehemu ya wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi<br><br>▪ Kamati ya Uchunguzi izingatie muda iliyopewa na Mamlaka ya Nidhamu na muda uliowekwa kisheria.<br><br>▪ Uchunguzi ufanyike kwenye mazingira ya faragha (in camera).<br><br>▪ Mtuhumiwa anayo haki ya kuhudhuria au kuwakilishwa na mtumishi mwenzake, wakili, au chama cha wafanyakazi wakati wa Uchunguzi.<br><br>▪ Mtuhumiwa anayo haki ya kuona, kuhoji na kupewa nakala za nyaraka za ushahidi dhidi yake. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kikao, majukumu, mipaka ya Kamati , haki za mtuhumiwa na jinsi Uchunguzi utakavyo-fanyika. | | | ▪ Katika mazingira ambayo Mwajiri siyo Mamlaka ya Nidhamu Mwajiri huyo ana haki ya kuhudhuria Uchunguzi au kuwakilishwa na kutoa maelezo |
| | ▪ Kurekodi mwenendo wa Uchunguzi (*mahojiano*)<br><br>▪ Kutembelea maeneo yanahusika na tuhuma (ikilazimu)<br><br>▪ Kuandaa taarifa ya Uchunguzi<br><br>▪ Kukabidhi mwenendo na taarifa ya Uchunguzi kwa Mamlaka ya Nidhamu | | | ▪ Ikiwa wakati wa Uchunguzi kuna ushahidi wa tuhuma mpya Mamlaka ya Nidhamu ijulishwe ili itoe Hati ya Mashtaka kwa tuhuma mpya.<br><br>▪ Mtuhumiwa akipewa Hati mpya, atatoa utetezi wake na Kamati ya Uchunguzi ipewe maelekezo ya kuendelea na Uchunguzi wa tuhuma mpya.<br><br>▪ Ikiwa shahidi muhimu hayupo siku ya Uchunguzi na ameahidi kuwepo ndani ya muda fulani, Uchunguzi uahirishwe hadi shahidi huyo atakapohudhuria.<br>▪ Ikiwa Kamati ilisahau kuchukua ushahidi kutoka kwa shahidi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | muhimu ambaye Kamati imeshamruhusu kusafiri nje ya kituo cha uchuguzi, Kamati iwezeshwe ili nayo imwezeshe shahidi huyo kuwasilisha ushahidi au kwa Kamati imfuate mahali alipo. |
| | | | | ▪ Taarifa ya Uchunguzi iandaliwe na Kamati ya Uchunguzi yenyewe bila kumshirikisha Mwajiri au mtuhumiwa.<br><br>▪ Kamati iwasilishe taarifa ya Uchunguzi ndani ya muda iliyopangiwa na Mamlaka ya Nidhamu.<br><br>▪ Uchunguzi umalizike ndani ya siku **sitini (60)** tangu ulipoanza.<br><br>▪ Ikiwa Uchunguzi (*katika mazingira fulani*) umeshindwa kumalizika kwa muda uliowekwa, Kamati iombe kwa Mamlaka ya Nidhamu kuongezewa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | muda ambapo itaongezewa muda usiozidi **siku thelethini (30).** |
| **KUHITI-MISHA HATUA ZA NIDHAMU** | ▪ Kupokea mwenendo na taarifa ya Uchunguzi<br>▪ Kuchambua na kutathmini Taarifa ya Uchunguzi | **Kanuni ya 19** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu-2016*) | Mamlaka ya Nidhamu | ▪ Taarifa ya Uchunguzi ieleze wazi kama tuhuma zimethibitika au la, na sababu zake.<br>▪ Kamati inaweza kutoa maoni kuhusu maelezo au ushahidi uliobainika kuongeza au kupunguza uzito wa kosa lililotuhumiwa (*Aggrevation and Mitigation factors*)<br>▪ Taarifa ya Uchunguzi ioneshe ushahidi wote uliotumika wakati wa Uchunguzi.<br>▪ Taarifa ya Uchunguzi isiwe na mapendekezo ya adhabu.<br>▪ Endapo Mamlaka ya Nidhamu itaona kuna upungufu wenye ulazima wa kurudia Uchunguzi, itoe maelekezo kwa Kamati kufanya Uchunguzi upya. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ▪ Kutoa uamuzi wa shauri<br><br>▪ Kumjulisha mtuhumiwa uamuzi wa shauri **(Kiambatisho "A")** | **Kifungu cha 13** (*Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu*)<br><br>**Kanuni ya 30** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu-2016*) | Mamlaka ya Nidhamu | **(a) Kwa mwenendo wa makosa mazito (*Formal proceedings*)**<br><br>• Mtuhumiwa na Mwajiri wajulishwe uamuzi wa shauri la Nidhamu na sababu za uamuzi huo ndani ya siku **thelathini (30)** tangu tarehe ya Mamlaka ya Nidhamu ~~kupokea taa~~rifa ~~ya Kamati~~ ya ~~Uchunguzi~~.<br><br>▪ Kushindwa kutoa uamuzi ndani ya siku 30 itatafsiriwa kuwa, **mtuhumiwa hana hatia ya kosa alilotuhumiwa**<br><br>▪ Endapo mtuhumiwa ametiwa hatiani, adhabu itolewe kwa kuzingatia kosa lililofanywa na Sheria au Kanuni iliyokiukwa.<br><br>▪ Barua ya uamuzi iwe na sababu za Mamlaka ya Nidhamu kufikia |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Uamuzi ilioufanya. |
| | | | | ▪ Kupitia barua ya uamuzi, Mtuhumiwa pamoja na Mwajiri wajulishwe haki, muda na mahali pa kukata rufaa iwapo hawataridhika na uamuzi.<br>▪ Barua za Uamuzi wa mashauri zipelekwe kwa Walimu husika na kuwe na ushahidi wa tarehe ya kupokea barua hizo. |
| | | **Kanuni ya 20** (*Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu-2016*) | Mamlaka ya Nidhamu (*ngazi ya Shule na Wilaya*) | **(b) Kwa mwenendo wa makosa mepesi (*Summary proceedings*)**<br>• Baada ya kupewa Hati ya mashtaka, Mwalimu akishindwa kuwasilisha / kutoa utetezi kwa maandishi au kwa mtazamo wa Mamlaka ya Nidhamu utetezi uliotolewa haukidhi, Mamlaka ya Nidhamu itaweka kumbukumbu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | kuwa mtuhumiwa amepatikana na hatia na itoe adhabu kuzingatia Jedwali la kwanza la Kanuni za Tume |

**JEDWALI LA 2:**

## MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA HATUA ZA NIDHAMU KWA MWALIMU ALIYEKABILIWA NA KESI YA JINAI MAHAKAMANI

| KANUNI | MAELEKEZO | HATUA ZA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **Kanuni za Tume, 21(a)** | Mwalimu amefunguliwa/ anakabiliwa na kesi ya jinai mahakamani kabla ya kufunguliwa shauri la Nidhamu | Shauri la Nidhamu halitafunguliwa hadi kesi ya jinai itakapohitimishwa |
| **21(b)** | Shauri la Nidhamu limefunguliwa na linaendelea dhidi ya Mwalimu na kabla ya kuhitimishwa Mwalimu anafunguliwa kesi ya Jinai. | Shauri la Nidhamu litasimama ili kupisha kuhitimishwa kwa kesi ya Jinai. |
| **21(c )(d)** | Kesi ya jinai imehitimishwa mahakamani na Mwalimu ameachiwa huru kwa **sababu za kiufundi** (*legal technicality*) | Kuachiwa huru kwa sababu za kiufundi hazizuii Mwalimu huyo kuchukuliwa hatua za kinidhamu. Shauri la Nidhamu linaweza kuanzishwa au kuendelezwa dhidi ya Mwalimu huyo hadi kupewa adhabu kana kwamba hakuwa na kesi ya jinai mahakamani. |
| **21(k)** | Kabla ya kukabiliwa na kesi ya jinai, Mwalimu alifunguliwa shauri la Nidhamu, alipatikana na hatia na alipewa adhabu. Baadae alifungulia kesi ya jinai na kutiwa hatiani kwa msingi wa hoja na mazingira ya ushaidi wa shauri la kinidhamu. | Itakuwa halali kwa Mamlaka ya Nidamu kubadilisha adhabu iliyotolewa awali kwa hatia ya kosa la kinidhamu, kwa kutoa adhabu nyingine ya kinidhamu inayofaa kwa kosa la jinai lililofanywa au kwa kuzingatia ushaidi uliotumika wakati wa kesi ya jinai . |

| KANUNI | MAELEKEZO | HATUA ZA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **21(e), Kanuni ya 39** (*Kanuni za Utumishi wa Umma,2003*) | Mwalimu ametiwa hatiani kwa kosa la jinai baada ya kesi ya jinai kuhitimishwa | • Mwalimu (anaweza) kusimamishwa kazi (Suspended) kupisha tathmini kama pia anayo hatia chini ya Kanuni za Tume za mwaka 2016.<br><br>• Mwalimu aliyesimamishwa kazi baada ya mahakama kumtia hatiani kwa kosa la jinai (hatalipwa mshahara) atalipwa posho isiyozidi theluthi moja ya mshahara wake kwa mwezi. |
| **21(f)(h) (i)** | Mwalimu akitiwa hatiani kwa kosa la jinai lenye uzito wa kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi, utakuwa ni ushahidi kuwa pia anayo hatia chini ya Kanuni za Tume za mwaka 2016 endapo mazingira ya kesi na mashtaka yaliyozingatiwa mahakamani yatafanana na itakavyozingatiwa na Mamlaka ya Nidhamu. | Hatua za kinidhamu hazitaanzishwa au kuendelezwa dhidi ya Mwalimu aliyekutwa na hatia ya kosa la jinai mahakamani .<br><br>**AU**<br>Hatua za kinidhamu zinaweza kuanzishwa au kuendelezwa dhidi ya Mwalimu huyo. |
| **21(g) (j)** na **23** | Mwalimu aliye na hatia ya kosa jinai asiadhibiwe bila kupewa Notisi inayoeleza:<br>(i) Kosa la kinidhamu ambalo pia ni kosa la jinai alilotiwa hatiani mahakamani<br>(ii) Adhabu inayokusudiwa kutolewa na Mamlaka ya Nidhamu<br>(iii) Muda wa Mwalimu (mtuhumiwa) kutoa utetezi wake | Mamlaka ya Nidhamu haitalazimika kutoa adhabu kubwa iliyoainishwa kwenye Notisi. Adhabu ndogo inaweza kutolewa/ kuzingatiwa.<br><br>Mamlaka ya Nidhamu itumie **Sampuli ya Notisi** (***Kiambatisho 'B'***) |
| **22(1)(a)(b)** | Kesi ya jinai itachukuliwa kuwa imehitimishwa endapo:<br>• Hakuna rufaa yoyote iliyokatwa ili kupinga kutiwa | Kama kuna shauri la Nidhamu, litaendelea kusimama kupisha mchakato wa rufaa |

| | | |
|---|---|---|
| | hatiani kwa kosa la jinai au kuachiwa huru na muda wa rufaa umemalizika.<br>• Kuna rufaa iliyokatwa (ndani ya muda wa rufaa) kupinga kutiwa hatiani kwa kosa la jiani . | ukamilishwe. |

**JEDWALI LA 3:**

## MAJUKUMU NA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA HATUA ZA RUFAA

| KAZI | HATUA ZA UTEKELEZAJI | REJEA | MTEKELEZAJI | MAMBO YA KUZINGATIA |
|---|---|---|---|---|
| **KUPOKEA RUFAA** | Kupitia barua ya rufaa na viambatanisho iwapo vinatosha kufanyiwa kazi kama rufaa (*Mfn. chunguza Muda wa rufaa)* | **Kifungu cha 13** (*Sheria ya Tume Na.25, 2015*) , **Kanuni ya 30** na **31**(*Kanuni za Tume, 2016*) | Maafisa wachambuzi wa rufaa (Tume Makao makuu na Wilaya) | Kuainisha na kutunza vielelezo |
| | Kusajili rufaa kwa "Track No." | | Sekretarieti /Katibu Msaidizi wa Wilaya | Namba za Ufuatiliaji (*Track Number*) zisifanane |
| | • Kumjulisha mrufani kuhusu kupokelewa kwa rufaa yake na upungufu wowote (kama upo) mfano mrufani aliyekata rufaa kutoonesha sababu za kukata rufaa/ au kukata rufaa nje ya muda wa siku 45 tangu tarehe ya (mrufani) kupokea barua ya uamuzi wa shauri lake. | **Kanuni ya 61(4)** (*za Utumishi wa Umma za 2003 )* | Sekretarieti /Katibu Msaidizi wa Wilaya | • Barua ya kumjulisha mrufani iandikwe mapema .<br>• Barua ya Rufaa iwe na tarehe ya kupokea uamuzi na sababu za kukata rufaa hiyo. ***Kiamb. "C"***<br>• Aidha barua ya rufaa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | iliyokatwa nje ya muda wa siku 45 ioneshe sababu za rufaa hiyo kukatwa nje ya muda. |
| | Kuomba taarifa ya mwenendo wa shauri kutoka Mamlaka ya Nidhamu na au Mwajiri | **Kanuni ya 30(3)** (*Kanuni za Tume ,2016*) | Maafisa wachambuzi wa rufaa (*Tume Makao makuu na ngazi ya Wilaya*) | Muda wa **siku 14** uliowekwa kwa Mamlaka ya Nidhamu uzingatiwe |
| **KUCHAM BUA RUFAA** | Kupitia sababu za rufaa na taarifa /maelezo ya Mamlaka ya Nidhamu, Mwajiri au Mrufani | | Maafisa wachambuzi wa rufaa rufaa (*Tume Makao makuu na ngazi ya Wilaya*) | Umakini na usiri katika uchambuzi |
| | Kufanya uchambuzi wa hoja na kuandaa maoni na mapendekezo ya rufaa kwa ajili ya kikao cha Menejimenti cha maandalizi ya Mkutano wa Tume/ Katibu Msaidizi (W) | | Maafisa wachambuzi | Uchambuzi na vikao vifanyike mapema |
| | Kufanya vikao vya maandalizi ya mkutano wa Tume | | Menejimenti | Vikao vifanyike kila baada uchambuzi wa rufaa kadhaa unapofanyika. |
| | Kuingiza masahihisho yaliyofanywa kwenye kikao cha maandalizi | | Maafisa wachambuzi | Masahihisho yaliyofanywa kwenye kikao cha maandalizi yazingatiwe. |

| KAZI | HATUA ZA UTEKELEZAJI | REJEA | MTEKELEZAJI | MAMBO YA KUZINGATIA |
|---|---|---|---|---|
| **KUHITI MISHA RUFAA** | • Kupitia uchambuzi wenye maoni na mapendekezo kuhusu rufaa<br>• Kuwasikiliza Mrufani/Mamlaka ya Nidhamu iliyomba kutoa utetezi mbele ya Tume<br>• Kutoa uamuzi wa Rufaa | **Kanuni ya 62(2)(3)** *(Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003* | Mamlaka ya rufaa<br>*(Makamishna wa Tume, / Kamati ya Wilaya )* | **Muda wa siku 90** uliowekwa kisheria uzingatiwe |
| **KUJULISHA UAMUZI WA RUFAA** | Kuandika barua za uamuzi wa rufaa uliotolewa na Mamlaka ya Rufaa. | **Kanuni ya 63** *ya Kanuni za Utumishi wa umma.* | Sekretarieti /Katibu Msaidizi - Wilaya | • Barua zioneshe iwapo rufaa ilikubaliwa au kukataliwa<br>• Barua zioneshe sababu za kufikia uamuzi huo<br>• Barua zioneshe haki ya mrufani kukata rufaa ngazi inayofuata ikiwa hataridhika na uamuzi wa rufaa yake.<br>• Barua za Uamuzi wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Rufaa zipelekwe kwa warufani na kuwe na ushahidi wa tarehe ya warufani kutumiwa/ kupokea barua hizo. |
| **KUTEKE-LEZA MAAGIZO YA MAMLAKA YA RUFAA** | • Kutekeleza uamuzi wa Mamlaka ya Rufaa<br>• Upande usiokubaliana na uamuzi ukate Rufaa kwa kuzingatia Kifungu cha 13 cha Sheria ya Tume, Na.25, ya 2015 | **Kanuni ya 64(1)** (*ya Kanuni za Utumishi wa umma, 2003)* | Mamlaka ya Nidhamu,<br>Mwajiri au<br>Mrufani. | Mamlaka au mtumishi anayekaidi kutekeleza uamuzi wa rufaa uliotolewa na Tume (TSC) au Rais anaweza kushtakiwa kinidhamu. |

***KIAMBATISHO "A"***

**(SAMPULI YA BARUA YA UAMUZI)**

Mwl...........................................................

S.L.P ........................................................

**K.k.** Mkurugenzi Mtendaji/wa Manispaa

H/Wilaya / Manispaa ya......................

S.L.P.................................................

**YAH: UAMUZI WA SHAURI LA NIDHAMU**

Tafadhali rejea Hati ya mashtaka ya tarehe ...................ambayo ilikufungulia Shauri la Nidhamu na kukutaka (kupitia Notisi) utoe utetezi, dhidi ya tuhuma kuhusu.....................................

Napenda kukuarifu kuwa, Kamati ya Wilaya katika Kikao chake Na. ................ kilichofanyika tarehe ............. hadi tarehe...............kilifikia Uamuzi wa Shauri lako ambapo **umepatikana / hukupatikana na hatia** kutokana na ushahidi ufuatao:-

(i) ..............................................

(ii) ..............................................

(iii) Taarifa ya Kamati ya Uchunguzi uliofanyika tarehe..............

(iv) Utetezi wako ulioutoa wakati unajibu hati ya Mashtaka ........na wakati unajitetea mbele ya Kamati ya Uchunguzi tarehe ..................................................................

(v) Nakala ya daftari la mahudhurio ambalo hukusaini kuanzia tarehe ..................... hadi ......................

Kutokana na hatia hiyo, Kamati ya Wilaya kwa Mamlaka iliyopewa na kifungu cha **12(1)(g)** cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 kikisomwa sambamba na Kanuni ya **47(a)** ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016, umetiwa hatiani kwa kukiuka Kanuni ya ……… ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016. Kwa hatia hiyo, umepewa adhabu ya ………………………… kwa mujibu wa Kanuni ya ………………… ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016 kuanzia **tarehe** …………hadi **tarehe**………

Endapo hutaridhika na Uamuzi huu, unayo haki ya kukata rufaa Tume ya Utumishi wa Walimu (Makao Makuu) Dodoma, ndani ya siku **Arobaini na tano (45)** tangu siku/tarehe ya kupokea barua ya Uamuzi huu. Haki hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha **13 (2)** cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, 2015 pamoja na Kanuni ya **30** ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, 2016.

**(Jina na saini)**
**<u>MAMLAKA YA NIDHAMU</u>**

***KIAMBATISHO "B"***

**(SAMPULI YA NOTISI)**

**OFISI YA RAIS**
**TUME YA UTUMISHI WA WALIMU**

**NOTISI**

*(Kanuni ya **21(g) (j)** ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za 2016)*

Bw/Bibi/Bi...............................Mwalimu (daraja/cheo) .............., TSD NA. ............., Mwajiriwa wa................Shule ya Msingi/Sekondari ya ........... S.L.P.........................................................................................

Nakujulisha kwamba, ninakusudia kuchukua hatua za Nidhamu dhidi yako kwa kukupa adhabu ya ................................ Kusudio hili linatokana na Mahakama (jina) iliyokaa tarehe ............... Mjini(mahali) ................ katika Kesi ya Jinai Na. .................. ya mwaka .................. iliyokukabili, ilikukuta na ***hatia ya kosa la*** ..................... Kutokana na hatia hiyo, inatafsiriwa kuwa pia umefanya kosa la kinidahmu chini ya Kanuni ya .................... ya Kanuni za Utumishi wa Walimu za mwaka 2016.

Kwa Notisi hii, unatakiwa kutoa utetezi wako kwa maandishi ukijibu kwa nini usipewe adhabu hiyo. Utetezi huo unifikie ndani ya ***muda wa siku kumi na tano (15)*** kuanzia tarehe ya kupokea Notisi hii.

Tambua kwamba, endapo utetezi wako hautanifikia katika muda uliotajwa hapo juu, kwa kuzingatia Kanuni ya **21(g)(ii)** ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016, nitaendelaea na taratibu za kukupa adhabu hiyo bila kukupa tena taarifa/notisi.

Tarehe _______________ ______________________________
Sahihi ya Mamlaka ya Nidhamu

.............................................................................................................

Nathibitisha kwamba, nimepokea nakala ya Notisi hii .

Tarehe_________ ______________________________
Sahihi ya Mwalimu Mtuhumiwa

**_KIAMBATISHO "C"_**

**(SAMPULI YA BARUA YA RUFAA)**

**Anuani ya Mrufani**
Simu....................
Tarehe...................

Katibu, / Katibu Msaidizi
Tume ya Utumishi wa Walimu
Makao makuu Dodoma / Wilaya ya.........
S.L.P 353
**DODOMA**

**YAH: RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA MAMLAKA YA NIDHAMU**

---

Husika na somo tajwa hapo juu.

Nakiri kuwa, tarehe .............nilipokea barua ya Uamuzi wa shauri la Nidhamu lililonikabili ambapo Mamlaka ya Nidhamu ( *taja jina na mahali Mamlaka ya nidhamu ilipo*) ilinitia hatiani na kunipa adhabu ya ...................................

Kufuatia Uamuzi wa shauri hilo, nimeamua kukata rufaa hii kwa **sababu** zifuatazo:-

1. ......................................
2. ......................................

......................................
**Jina na saini ya Mrufani**

***KIAMBATISHO "C"***

**(SAMPULI YA BARUA YA RUFAA)**

**Anuani ya Mrufani**
Simu....................
Tarehe...................

Katibu, / Katibu Msaidizi
Tume ya Utumishi wa Walimu
Makao makuu Dodoma / Wilaya ya........
S.L.P 353
**DODOMA**

**YAH: RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA MAMLAKA YA NIDHAMU**

---

Husika na somo tajwa hapo juu.

Nakiri kuwa, tarehe .............nilipokea barua ya Uamuzi wa shauri la Nidhamu lililonikabili ambapo Mamlaka ya Nidhamu ( *taja jina na mahali Mamlaka ya nidhamu ilipo*) ilinitia hatiani na kunipa adhabu ya ................................

Kufuatia Uamuzi wa shauri hilo, nimeamua kukata rufaa hii kwa **sababu** zifuatazo:-

1. .........................................
2. .........................................

.......................................
**Jina na saini ya Mrufani**